

  
**OFISI YA RAISI,  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI**

**SHULE YA SEKONDARI MENGELE**

**OFISI YA MKUU WA SHULE**

**S.L.P 145, CHIMALA**

SIMU: 255759817548

Tarehe 06 DISEMBA 2020

Kumb.Na.MSS/JI/Vol.01

MWANAFUNZI: .....

SHULE YA MSINGI: .....

S.L.P:.....

**CHIMALA-MBEYA.**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MENGELE KIDATO CHA KWANZA  
MWAKA .....**

## **1.0. UTANGULIZI:**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule hii. Nakupongeza kwa kupata nafasi hiyo. Ni matumaini yangu kuwa utaitumia fursa hii vizuri kusoma kwa bidii na kuongeza maarifa zaidi kwa manufaa ya maisha yako ya baadaye, familia yako na Taifa zima kwa ujumla. Aidha ni tegemeo langu pia, kuwa utakuwa na nidhamu nzuri na utatekeleza na kufuata sheria na kanuni zote za shule hii pamoja na masharti yote ya kujiunga kama yalivyo orodheshwa katika fomu hii. Shule hii ni shule ya kutwa kwa kidato cha I- IV na ni mchanganyiko. Vile vile ina kidato cha V-VI. Kidato cha tano na cha sita ni wasichana tu na hukaa bweni. Masomo yote hufundishwa kwa kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili, hivyo basi Shule imetenga muda maalumu kwa ajili ya mafunzo ya Kiingereza (English Orientation Course) kabla ya kuanza rasmi masomo yote. Aidha ni wajibu wako kuhakikisha unafanya jithada kubwa kujifunza somo la Kiingereza ili uweze kumudu vema masomo mengine. Shule ipo Kata ya Chimala katika Wilaya ya Mbarali mkoza wa Mbeya kilometra 60 kutoka zilipo ofisi za Halmashauri ya wilaya ya Mbarali, kando ya barabara iendayo Dar es salaam. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021**, Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **25/01/2021**. Unatakiwa kufika siku shule itakapofunguliwa pamoja na Mzazi/Mlezi

## **2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

### **2.1. SARE ZA SHULE**

- a) Rangi ya sare za shule hii ni Kijani Jeshi na Light Blue kwa wavulana na wasichana (vipande vya kitambaa vimeambatanishwa).
  - i. Wavulana suruali mbili na tai mbili. Suruali isiwe ya mlegezo na wala isiwe ya kubana (modo)
  - ii. Wasichana sketi mbili na tai mbili. Sketi ziwe ndefu kupita magoti na zisiwe za kubana. **NB: Sketi ifike kwenye kifundo cha mguu (Karibu na unyayo).**
- b) Mashati mawili meupe ya mikono mifupi kwa wasichana na wavulana. Shati moja liwekewe nembo ya kijani jeshi na lingine light blue kwenye upande wa kushoto wa kola.
- c) Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vinavyofunika miguu na viwe vya visigino vifupi.
- d) Soksi nyeupe jozi mbili kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana. Kwa wasichana soksi ziwe ndefu.

- e) Sare za michezo
  - i) Raba jozi moja na Tshirt ya Blue kwa wavulana na wasichana
  - ii) Bukta ya blue kwa wavulana na track suti ya blue kwa wasichana.
- f) Kwa wasichana wa Kiislam. Hijabu nyeupe na nusu kanzu tetroni isiyangaza pamoja na sketi ndefu inayofika kwenye kongo mbili za miguu.
- g) Sweta moja rangi ya kijani kibichi kwa ajili ya kipindi cha majira ya baridi.

## 2.2. VIFAA VYA KITAALUMA

- a) Begi moja rangi nyeusi kwa ajili ya kubebea madafatri.
- b) Madaftari makubwa (counter books) yasiyopungua 10.
- c) File mmoja la kutunzia kumbukumbu zako.
- d) Mkebe mmoja wa Hisabati (Mathematical Table) na vifaa vyake.
- e) Peni/kalamu za kutosha.
- f) Rula moja urefu wa m 30.

## 2.3. CHAKULA CHA WANAFUNZI WA KUTWA

### MAHITAJI YA CHAKULA MWAKA 2021

Mwanafunzi anapoletwa shule aje na vitu vifuatavyo kwa ajili ya chakula chake.

1. Mahindi yaliyokobolewa debe 2 kwa mwaka.
2. Maharage kablanketi debe 2 kwa mwaka.
3. Chumvi kilo 1 (paketi 2 kwa mwaka).
4. Mafuta ya kula (kupikia) lita 5 kwa mwaka.
5. Sukari kilo 5 kwa mwaka.
6. Tsh. 20,000/= (kwa ajili ya kuni, mpishi, kusaga, usafiri, sufuria na mbogamboga)

**NB: Kamati ya chakula ya wazazi itahusika na ukusanyaji wa michango yote.**

Mahitaji yote hayo ni makadirio kwa mwaka mzima, hivyo kwa muhula wa kwanza utatakiwa kuleta nusu ya kila ulichoambiwa (kuanzia namba 1 hadi 5) na ulete wakati unaripoti shulen. Na kiasi cha 20,000 (namba 6) kilipwe unaporipoti, kiasi hiki hakina nusu. Aidha kutakuwa na vikao vya wazazi/walezi kila baada ya miezi mitatu vitakavyokuwa vinaitishwa na kamati ya chakula ya wazazi ili kujua mwenendo wa chakula.

## 2.4. MAHITAJI MENGINE YA KIBINADAMU

Mwamvuli mmoja au koti la mvua (kwa majira ya mvua), ndoo ndogo moja na fagio moja la chelewa.

## 3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

3.1. Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenyeye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenyeye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulen.

- a) Heshima kwa **walimu, viongozi, wazazi, wafanyakazi wote na viranja wa shule, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla** ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) Kuwahi kufika shulen na katika kila shughuli za shule na nyinginezo utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maeleo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha mkuu wa shule ni kosa.

- f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule. Mwanafunzi anatakiwa kuoga kila siku, kukata nywele na kuzichana, kukata kucha, kupiga mswaki kila siku, kunyoa ndevu na kuvalaa vizuri wakati wote. Mitindo ya rasta, kalkiti, panki, kusuka, kutinda nyusi au kunyoa vipara hairuhusiwi kabisa. Aidha ni marufuku kuvalaa mapambo kama vile mikufu, hereni, bangili, shanga, kofia, kupaka rangi kucha, wanja, rangi za midomo, kuvalaa pete nk.
- g) Kuvalaa sare za shule wakati wote unapotakiwa. Sare fupi (sketi/suruali/shati zenyenye kubana haziruhusiwi kabisa).
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- i) Kutunza mali za umma.
- j) Kusimama na kusalimu walimu, wafanyakazi wote na wakubwa wanapopita ama kuongea nao.

### **3.2. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.**

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli nk.
- e) Makosa ya jinai
- f) Kupiga au kupigana
- g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- h) Kudharau bendera ya Taifa
- i) Kuoa au kuolewa
- j) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule
- k) Kutoa mimba
- l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- m) Kukataa adhabu kwa makusudi
- n) Kuwa na simu ya mkononi
- o) Kutembea, kushiriki na kwenda sehemu zifuatazo; **vilabu vya pombe, majumba ya starehe na nyumba za kufikia wageni.**
- p) Kutukana au kutumia lugha chafu.

### **4.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.**

- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shulenii.
- b) Fomu ya maelezo kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

### **5.0. ZINGATIA**

- a) Tafadhalii soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.
- b) Mara tu mwanafunzi anaripoti shulenii aingie ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule kwa ajili ya kusajiliwa/kudahiliwa (Admission).

**NAKUTAKIA MASOMO MEMA  
KARIBU SANA MENGELE SEKONDARI UFUTE UJINGA**

.....  
**PASKALIA . E. MAGANGA  
MKUU WA SHULE**

## OFISI YA RAIS-TWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

### **A: TAMKO LA MWANAFUNZI KUKUBALI MAAGIZO NA KUFUATA SHERIA NA KANUNI ZOTE ZA SHULE**

(Ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)

Mimi ..... niliyechaguliwa kuijunga na kidato cha kwanza mwaka ..... Katika Shule ya Sekondari Mengele. Nimesoma na kuelewa sheria na kanuni zote zilizoandikwa. Ninakubali kuijunga na shule hii na ninaahidi kufuata sheria na kanuni zote za shule kwa wakati wote nikiwa mwanafunzi. Pia ninaahidi ya kwamba nitahudhuria shule siku zote za masomo na sitashiriki au kujihusisha katika migomo, fujo, makosa ya jinai na katika makosa yote yanayoweza kunifukuzisha shule.

### **B:TAMKO LA MZAZI**

Mimi ..... Mzazi/Mlezi wa .....  
aliyechaguliwa kuijunga kidato cha kwanza mwaka ..... Katika Shule ya Sekondari Mengele.  
Nimesoma na kuyaelewa maagizo, sheria na kanuni za shule.

Ninaahidi ya kwamba nitatekeleza maagizo yote ambayo yameainishwa katika fomu hii, ikiwa ni pamoja na mahitaji ya mwanafunzi wakati akijiunga na shule. Ninakubali/Sikubali kumtimizia mahitaji yake yote kama yalivyoanishwa na ninaahidi kuwa karibu naye ili kujua mwenendo wake kitaaluma , kinidhamu na pia kujua mahitaji yake.

### **MAWASILIANO**

1. .....
2. .....

Mahusiano (weka ✓)

Baba  , Mama  , Bibi  , Mjomba  , kaka  , dada  , mengineyo  (taja).....

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
MINISTRY OF EDUCATION , SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING  
**FORM 1**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

MENGELE SECONDARY SCHOOL,

P.O BOX 145,

**CHIMALA-MBEYA.**

DATE ...../...../20.....

REF: NO.MSS/MEF/Vol.01  
MEDICAL OFFICER,

**PART I**

**REF: FORM ONE ENTRANT.....**

AGE ..... YEARS ..... SEX .....

Please examine the above named form one entrant as to his/her physical and mental fitness to pursue secondary education at this school. The examination should include the following categories:-

1. Hemoglobin .....
2. P.V Bleeding .....
3. Sight .....
4. Blood pressure .....
5. Urine analysis .....
6. Stool examination .....
7. Pregnancy test .....
8. Skin diseases .....
9. Leprosy .....
10. Any deformity .....
11. Epilepsy .....
12. Pulmonary tuberculosis .....
13. Neurosis .....
14. Venereal diseases .....
15. Eye test .....
16. Ears .....
17. Chest .....
18. Spleen .....
19. Abdomen .....
20. Other diseases eg: physical defects or impairments infectious/chronic/family diseases .....

**PART II**

1. I have examined the above named form one Entrant and I certify that he/she is physical and mental fit/unfit to pursue secondary education studies.
2. Other comments .....

Signature .....

Designation .....

Station .....

Date .....

Official stamp .....

NB: No student will be enrolled without certification of his/her physical and mental fitness.